

## ANDANENGA ASIFIWE

1. Haki haiwi batili, ahusikae apewe  
Japo iwe na akali, mwenye haki asinyimwe  
Aipewe bikiuli, kwa nderemo si mayowe  
Andanenga, asifiwe, ameshinda kihalali.
2. Ameshinda kihalali, Andanenga asifiwe  
Ni mtunzi taamuli, wa komeo na kumewe  
Mahiri mwenye adili, hahitaji mizozombwe  
Andanenga, asifiwe, ameshinda kihalali.
3. Sifa anastahili, hana budi apongezwe  
Usifanye ubakhili, kuitia visandewe  
Kusema lile na hili, kama mcheza msewe  
Andanenga, asifiwe, ameshinda kihalali.

*M. M. S. Mziwanda (Hayanimbi)*  
*S. L. P 74,*  
*Shinyanga*